
السلفيون والشيعة / السواحلية

SHEIKH HASAN MUSA SAFFAR

# UHUSIANO BORA KATI YA

# SALAFI NA SHIA



# UHUSIANO WA MAFUNGAMANO BORA KATI YA SALAF (SUNNI) NA SHIA

I

Sheikh Hassan Saffar

**YALIYOMO**

UTANGULIZI........................................................................ i

MWANZO........................................................................ 1

JE UHUSIANO UNAENDELEA VIZURI?.................................... 5

MFANO WA UHUSIANO KATI YA SALAF NA SHIA................ 10

MASHUHUDIO NA KUATHIRIWA MOYO KWA MAZURI...... 13

HAKUNA JAMBO KAMA KUISHI PAMOJA KWA MAISHA YA AMANI........................................................................ 20

MJADALA, MAHALI PA MAKUBALIANO................................ 22

## UTANGULIZI

Watu wengi huenda wakayaweka mbali mawazo yao juu ya uwezekano wa kuwepo kwa uhusiano mzuri baina ya Salaf na Mashia. Hayo ni kwa ajili ya kuhitilafiana pande mbili hizi katika mambo ya ki akida yaliyo nyeti, na pia kwa kuwepo kwa historia iliyojaa mizozo na uhasimu baina ya makundi haya mawili. Na kwa ajili ya kuwa kikundi cha Salaf kina tabia ya kuwa na msimamo madhubuti kwa yale wanayoyaona yanahitilafiana na akida yao. Sio kwa kuwatazama Mashia tu bali hata ndani ya usunni.

Lakini sasa ninahisi kuwa kuna tamaa na matarajio juu ya hili. Kwani ndani yake mna maendeleo ya kifikra za kielimu zinazolengwa na kutarajiwa na makundi mbali mbali ya Kiislamu. Fikra hizi zinayafanya makundi haya kuwa karibu kukubaliana kwa kuwepo maoni mengine, na kuyatendea kazi mbali na tofauti kubwa zilizopo kati yao. Pamoja na kuwa kila kundi ni lenye kufuata misingi yake.

Kama vile kuwepo kwa mapambano makubwa ambayo yanawakabili umma, inapaswa kwa wale wenye busara katika pande zote mbili kuondoa tofauti hizi, ikiwa sizote basi hata kama ni kidogo. Na katika kukutana kwangu na kuwa na mafungamano ya karibu na wanavyuoni, waenezaji dini, wajuzi wa fani mbali mbali katika ndugu zangu wa Salaf, nimehisi dalili nzuri kwa njia hii, ambazo zinawafanya wawe na pupa juu ya maslahi ya dini na nchi yao. Na zinazo wazindua juu ya hatari iliyoenea inayowakabili umma kwa jumla.

Na katikati ya Ushia mna matayarishi kwa wanavyuoni wengi na wenye busara kwa kila hatua itakayoleta ushirikiano na umoja na kusaidia juu ya kujenga umoja wa nguvu (*harmony*).

Kinachohitajika ni kwanza kuchukua hatua za dhati zilizo na nguvu ambazo zitaweza kushinda ile nguvu ya wale walio na msimamo mkali katika pande zote mbili (Salaf na Ushia). Ile nguvu ambayo huenda ikahamasisha hisia za watu kwa

kuanza kuhitilafiana na kuzuia haraka ya kuleta umoja na ushirikiano na pia kuwatuhumu wenye kuleta mapatano kuwa wako mbali na akida.

Hakika watu wengi leo ni wenye kujiandaa sana kuliko nyakati zote zilizopita juu ya kulingania umoja na kuelekea wenye kuleta suluhu na wenye busara, jambo ambalo misimamo yake iko mbele ya pingamizi. Na pia vile vile kufanya juhudi ya kutosha ya kueneza busara na elimu inayofaa. Hili ndilo jambo ninalolihisi na kuliona na ninaenda mbio kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu ili nilifanya kuwa kweli kwa umma wote na ulimwengu. Kwa kusaidiana na wenye nia safi na wenye busara.

Hassan Saffar

24 Dhul Qaad'ah 1424 (A.H).

16 Januari 2004(A. D. Qatif)

# MWANZO

Historia yetu ya Kiislamu iliyo ndefu imeshuhudia vita na mizozo mingi ya kifikra na kimadhehebu. Na ambayo imeshuhudia kukosekana kwa amani katika jamii. Na pia kuzusha vita vya kijamii wakawa wanasiyasa ni wenye kuchangia zaidi jambo hili, kukawa na nguvu kutoka ndani yetu na kutoka nje zinazochochea mizozo hii na kufanya jamii kujihusisha na mambo yao ya kimisingi na kuzitumia nguvu zao kupambana wenyewe kwa wenyewe. Wakawa wameshindwa kukabiliana na nguvu zinazowatawala.

Na kukawa kujitenga kimadhehebu na kuyakubali maoni haya na kuyapinga mengine ndio kama ghala ya kuweka mizozo hii na uhasama.

Ama kuwepo madhehebu mingi na kuhitilafiana kwa maoni hilo ni jambo la kawaida lisiloweza kuepukika wala halina ubaya. Iwapo halitaleta ndani yake utengano wa chuki, na kuwepo na u imla wala uadui wa kimawazo.

Hakika umma wetu huu wa Kiislamu umepowa kutokana na majeraha ya utesi wa kifikra na kimadhehebu yaliyopita katika historia kama mzozo baina ya Jabriya (*Fatalism*) na Qadiriya, na kati ya Murjiah na wapinzani wao, na kati ya Ashaira na Mu'tazila na yale yaliyozuka juu ya kuwa Qur'an ni kiumbe au ni kitu kilicholetwa. Na pia mizozo baina ya madhehebu ya wanavyuoni wa fiqhi kama ile ikhtilafu baina ya dhehebu la Hanafi na Shafi, Hambali na Hanafi na baina ya dhehebu la Shafi na Hambali.

Mizozo hii ilikuwa mikubwa katika karne zilizopita, lakini sasa imepitwa na wakati katika vitabu. Mambo haya yana athari za kifikra na kijamii katika kuyapanua madhehebu hayo. Lakini kwa sasa hayaleti mgawanyiko mkubwa wala tofauti zenye chuki.

Na umebaki upinzani baina ya UShia na USunni kama mfano wa mwanya mkubwa katika ukuta unaozunguka umoja wa jamii ya Kiislamu. Mwanga huo unapulizwa na upepo wa

fitna na kupenya ndani yake malengo ya maadui na maelekezo yao.

Na wamefanya wanavyuoni wa Kisunni na Kishia wa karne hii juhudi juu ya kuuziba mwanya huu wa hatari uliobakia katika kupingana kimaneno na kifiqhi.

Na katika juhudi hiyo kulibuniwa chuo cha kuyaleta karibu madhehebu yote ya Kiislamu huko Cairo, Misri katika miaka ya hamsini na kuanzishwa mazungumzo ya kuleta umoja bila ya kulemea upande wowote. Na kuondoa mizozo ya kuhitilafiana katika ijtihada kiakida na kifiqhi.

Na kwa ajili ya juhudi hiyo imeweza kupunguza makali ya kutofautiana baina ya makundi ya haya mawili. Na kukawa na uhusiano mzuri baina ya sehemu zenye busara katika makundi mawili haya. Na yakawa yanashirikiana kwa pamoja juu ya kuleta maslahi ya hali ya juu kwa umma.

Na yale yaliyowezesha matarajio ya jamii kuondosha tatizo hili, sio kwa ajili ya kuridhika kundi moja kwa maoni ya kundi jengine na kujiondoa katika kuhitilafiana huku, bali ni kwa sababu ya misingi ifuatayo.

1. Kuanzishwa kwa chuo kikuu cha mafunzo ya Kiislamu kwa kuchanganya pande zote mbili.
2. Kuheshimiana na kwa sawa kwa pande zote mbili.
3. Kutegea njia ya mjadala katika kufanya mambo wanayotofautiana.
4. Kushirikiana na kusaidiana kwa pamoja juu ya kuleta maslahi kwa Waislamu na Uislamu kwa jumla.

Lakini kuna baadhi ya fikra za uchochezi zilizosimama kati ya Ushia na uSunni ambazo zimetatiza fikra hii ya kuleta umoja na kuidhohofisha mipango yake. Na katika athari zilizo mbele ni: Kusababisha maradhi mabaya (convulsion) yaliyosimama kuharibu uhusiano baina ya Salaf na Shia.

Na linatambulika dhehebu hili kwa kuwa na misimamo thabiti juu ya rai za wengine hata ndani ya madhehebu ya uSunni, hasa katika mambo ya akida. Kwa sababu hiyo ndio likawa linapinga harakati ya kukurubiana baina ya Sunni na Shia. Na ameandika mwanachuoni Nassir bin Abdillahi al-ahifari juu ya masuala ya kupima baina ya Ahli Sunna na Shia. Utunzi huu uko katika mijalada miwili. Na imefanywa chapa zaidi ya mara mbili huko Saudi Arabia. Akagusia ndani yake kwamba: "Harakati hiyo ya kukisia na kufanya karibu baina ya uSunni na Shia kwamba ni uzushi mkubwa unaotaka kuupa ukafiri na upotovu sifa ya sheria na jina la Uislamu. Na imesababisha harakati hiyo hasara kubwa kwa wafuasi wa Sunna na kuleta madhara yasiyokisiwa katika makabila na watu binafsi. (Kitabu: ***Al-Qafari*** cha Dkt. Nasir din bin Abdalla bin Ali, kuhusu mkuruba wa Sunni na Shia. Kifungu cha 2. Uk. 278 Chapa 6 Mwaka 1420 (A.H.) Daru Tayyiba, Riyadh)

Hayo ni maneno mageni na yenye kushangaza. Inadhihiri kwamba sababu ya kupinga harakati hii na kuohofia watu wa Sunna wasije wakaathiriwa na Ushia. Basi mbona isiwe kinyume? Kwani vile vitu vidogo ndivyo vinapasa kuogopa visije vikayayuka ndani ya habari kubwa iwapo havitakuwa vimejiweka madhubuti.

Na kabla ya miaka arubaini wakati wa kuanzishwa harakati hii ya kukurubisha baina ya Sunni na Shia, Ibrahim Sulaiman al-Jab-haan aliandika kitabu dhidi ya harakati hii na kukieneza. Kitabu hiki kilikuwa ni kwa unuani "Kuutenga upotovu na kuwazinduwa waliolala" katika kitabu hiki alifikia hadi kuwashambulia viongozi wa kizazi cha mtume (s.a.w.w.) (ahlul bayt) pindi aliposema katika utangulizi kitabu chake: "Hakika nimelifuatanisha jina la Jaffar bin Muhammad na alama ya kuuliza pasipo mahala pake, kwa ajili ya kurekebisha makosa yaliyoenea miongoni mwa waandishi wingi kwa kuliunganisha neno la (As-sadiq) mkweli kwa jina lake na kulifanya kama jina lake la kubandikwa (*lakab*) na kutambulika kwalo. Lakini kwa hakika jina hili au utakaso

huu haumstahiki mtu ambae amezingirwa na mambo yaliyo na shaka na kukawa na maneno mingi juu yake na alietengemezwa maneno yaliyojawa na ukafiri na upotovu." (***Al-Jab-hani:*** Ibrahim Suleiman Juz. 1 Uk. 8)

Kwa ushahidi hakika maneno haya hawayaridhii wafuasi wa Salaf, na wala Muislamu yeyote.

Katika kukabiliana kimejibu kitengo cha Ushia kwa kutunga vitabu na kuchapisha kwa kushambulia upande wa Salaf chini ya unuani (uwahabi). Na hili ni jina wasilolipenda wafuasi wa Salaf wao wenyewe.

## JE! UHUSIANO UNAENDELEZA VIZURI ?

Bila shaka kuna kitu cha hatari kinachoukabili umma wa kiislamu kwa wakati huu NI kisichokuwa na mfano katika historia iliyopita. Na dhehebu la Salaf ndilo lililo katikati ya kitu hiki cha hatari. Hilo ni kwa sababu baadhi ya vitendo vinavyotokana na wao ndivyo vilivyozuwa kitu hiki cha hatari.

Hakika ni jambo lisilotiliwa shaka na akili kuwa maradhi haya mabaya na mizozo iliyomo katika jamii yanavunja uwezo wa jamii katika kukabiliana na mapambano haya makali. Na pia kurahisisha fursa kwa maadui kuchezea na kuyaendesha wanavyotaka mambo haya yanayoleta mizozo. Kwa ajili hiyo hakika kunyoosha mkono kwa ajili ya kusaidiana kwa upande wa Salaf kuulekeza kwa madhehebu mengine ya kiislamu ndilo jambo lililo mbele katika akili na sheria. La sivyo watakuwa wamebeba udhaifu juu ya upinzani unaoendelea.

Jee sio jambo la kustaabisha tunapoona hatua za kuendelea na kushirikiana kati ya Mayahudi na Manasara! Na hizo ni dini mbili zilizokataliwa na kupingwa (na dini ya kiislamu). Na kuna tofauti kubwa kati yao za ki akida na mizozo mikubwa ya kihistoria. Lakini mbali na hayo, wameyapuuza mambo hayo na kushirikiana juu ya kuipuka hatari inayowakabili wote wawili. Kinyume na sisi Waislamu kuwa tunashindwa kuziondoa tofauti zetu na kushindwa kujiweka karibu karibu, na ambapo sisi sote ni dini moja tunaomfuata Mtume mmoja (s.a.w.w.). Na ambapo tunauwezo mkubwa wa kuondoa tofauti hizi na hatari hii inayotukabili iwapo tutaungana?

Na katika mwisho wa maelezo juu ya kuungana baina ya Mayahudi na manasara: Ni kama vile ilivyonukuliwa na majarida na mashirika ya habari kutoka kwa warsha ya kimataifa ya mapadri wa kiKatoliki na viongozi wa kiyahudi iliyofanywa mjini New York kwa muda wa siku mbili. Ambapo walikutana karibu mapadri kumi wa dhehebu la kiKatoliki na viongozi sita wa kiyahudi ni pia kuhudhuriwa na

wa wazungu wa Ulaya na wa Amerika na pia Waisraili wengine. Walikubaliana kushirikiana juu ya kukabiliana na uadui mkubwa unaoenea katika bara la Uropa. Yaani kukabiliana na ujambazi unaowakabili Mayahudi. Na waliisifu warsha hii wale waliohudhuria ya kuwa ni ya kufana zaidi katika historia. Kwani nyengine zilikuwa ni zenye mvurugano na kutokuwa na nidhamu kati ya pande mbili hizo. Na pia waliweza kubainisha njia zitakazo wawezesha kuwa na ufahamu mzuri juu ya dini.

Haya yalikuwa baaada ya kukutana rasmi John Paul na viongozi wawili wakubwa wa kiyahudi huko Roma. Na ukatilia mkazo mkutano huu juu ya kuyalinda na kuyahifadhi mazungumzo haya ya Mayahudi yanayolenga kuwaleta pamoja baina ya Mayahudi na Manasara. Na ulifanyika mkutano huu kufuatia misingi iliyobuniwa na John Paul wa pili katika miaka 25 iliyopita.

Na akaeleza kasisi wa ufaransa na mzungumzaji wa kundi la kiKatoliki (Patrick Dipo) kwa mkutano huo haujawahi kutokea namna yake.

Na akasema Naibu wa mwenyekiti wa kusimamia mambo ya Mayahudi (Alan Shtambrog) mkutano huu ndio mkubwa na wenye kukamilisha mjadala baina ya Katoliki na Mayahudi kwa ujumla.

Na wengi walipendekeza yakuwa kufanywe mikutano kama hiyo katika sehemu mbali mbali miaka ijayo. Na wakaahidi kwamba watakuwa ni wenye kuihimiza mijadala baina ya jamii ya dhehebu la kiKatoliki na Mayahudi. (***Al-Hayat.*** Gazeti la kila siku, London tarehe 22/1/2004 (A.D.)

Hivi ndivyo wanavyokwenda mbio wenzetu juu ya kushirikiana. Lakini sisi Waislamu tumelikosa jambo hilo la kutuondolea mizozo mbali na kuwa ni wenye kulihitaji zaidi jambo hilo la kushirikiana.

Hakika kutazama kwa makini upande huu wa kisiasa na

mbinu zinazohitajika na hali iliyopo ni jambo linalostahiki kutazamwa kwa makini na kufanyiwa upekuzi upande wa ndugu zetu wa Salaf kihukmu (sheria) na kimaudhui.

Na pahali sahihi pa kupata suluhisho la mambo haya ni Qur'an na Sunna. Ama maoni ya baadhi ya wanavyuoni kama vile ibnu Taimiyah na wengine pamoja na kuheshimiwa kwao, maoni yao ni katika kujitahidi na huenda yakakubaliwa au kukataliwa. Na huenda marejeo ya kupata dalili ya maneno kutoka katika Qur'an na Sunna yanayotokana na wanavyuoni na viongozi wa kiSalaf wa sasa, yanafungua njia mpya katika kugeuza na kubadili msimamo huu thabiti wa maoni ya wengine. Haya ni kwa upande wa sheria.

Ama kwa upande wa maudhui, ni kuwa sheria juu ya kitu huwa inatolewa kulingana na sura ya kile kitu. Kwani sheria (hukmu) kutoka kwa wanavyuoni waliopita wa Salaf.

Ama kwa upande wa maudhui ni kuwa hukmu ya jambo ni kama matawi yanayotokana na fikra za jambo hilo. Kwani hukmu za maulama wa Salaf waliotangulia ziko tofauti ni mielekeo mbali mbali. Miongoni mwao pia ni Mashia, imekuwa natija ya mawazo yao na kurekebisha kwao mambo ni kuondosha tofauti hizo. Na kupatikana vipenyo kwenye mawazo hayo na urekebishaji huo ni jambo ambalo lipo. Ima kwa sababu ya upungufu wa kufahamu kwa undani kundi jengine au kuchanganyisha mambo juu ya ufahamu wa maoni ya kundi hilo. Au kukubali baadhi ya maoni na kuyafanya ni ya watu wote.

Kwa mfano mfumo wa kifikra uliokuwa ukiongoza na kusifika mbele ya wanavyuoni wa Kishia zama zilizopita ni: wa Ikhbariyah ambao maelezo yake yako kwenye vitabu vine kama kitabu cha "*Al-Kaafi*" cha Kuleyni. Na kitabu cha *Tahdhib wal-istibsar*" cha Sheikh Tusi. Lakini nadharia ya Ikhbariyah ilififia sana na kuchukua uongozi ile ya *al-usuliyyah* kwa muda wa takriban karne tatu ambapo hatuyaoni kamwe yale yote yaliyokuwa yamepokewa kwenye vitabu vine bali yamebaki makejeli tu.

Na mfano mwengine unaofungamana na yale wanayoyachukulia maSunni na Salaf juu ya Mashia kuhusu kuwatuhumu makhalifa wane.

Basi kama jambo hilo lipo katika vitabu vya Mashia na vile vilivyopita basi huenda likawa ni natija ya hali waliokuwa wakiishi wakati huo kutokana na uovu na kutotendeana uadilifu. Lakini ukweli wa matendo kwa Mashia ni kuwa wako mbali na mfano wa mambo kama hayo. Kama mfano wa Mashia wa Iran ambao umekuwa uongozi upo chini ya wanavyuoni wao kwa muda wa miaka 25, na nchi yao ikawa ndio yenye nguvu, isipokuwa njia za kuelezana, na mawaidha ya kuwaleta wao pamoja yaliyopita na upepo. Na pia maneno ya viongozi wao hayakunufaisha chochote katika upande huo hata katika kilele cha kufanyiana uadui na wairaqi.

Hali hiyo pia ni vile vile kwa Mashia wa Lebanon ambao ni wenye nguvu na uwezo huko na ushindi mkubwa walioupata juu ya maadui wa ki Zionist. Isipokuwa tu njia za kuwajuza hazikuwakinga wao na chochote juu ya kuwakosea makhalifa na maswahaba watukufu pamoja na kina mama wa waumini.

Hakika katika jambo hilo mna ushahidi wa wazi wa kujitenga Mashia wa leo na makosa waliyokuwa wakiyafanya baadhi yao wakati uliopita.

Na huenda kukawa mna baadhi ya watu binafsi kati yao wanaoathiriwa na baadhi ya maoni na misimamo iliyopita (ya kuwakosea sahaba). Lakini tendo lao hilo haliwezi kuwachanganya wengine walio sawa. Hii mitazamo yote na mifano yake inawahitaji viongozi wa leo wa Salaf kuangalia kwa makini juu ya msimamo wao na fikra zao juu ya Mashia na pia vikundi vyengine vya kiislamu. Na kujiepusha juu ya kuzidisha mambo na kuyashikilia kwa nguvu. Na kufanya kwa ajili ya umoja wa Waislamu na kujiepusha na kutiana kwenye ukafiri na dhuluma na kudhaniana mabaya kwa yeyote katika Waislamu.

Na huenda kukawa na rai na maoni mengi na miongoni yanayowaongoza katika zama hizo lakini yaliendelea na

kubadilika baadae. Mambo haya yote yanapaswa kuwapelekea wafuasi wa leo wa Salaf kuwasoma Mashia wa leo katika maoni yao na miongozo yao.

## MFANO WA UHUSIANO KATI YA SALAF NA SHIA

Nimepitia kitabu kipya kilichotolewa mwezi huu cha Imam Sheikh Muhammed Mahdy Shamsuddin (r.a.) (aliekufa mwaka 1421 H) kitabu hicho ni kwa jina (hukmu za ujirani katika sheria ya kiislamu). Nacho ndicho kitabu chake cha mwisho kuandika alipokuwa katika maradhi yake huko Paris punde tu kabla ya kufariki. Nikaangalia katika utangulizi mrefu wa kitabu (uk 17) ulioandikwa na Sheikh Zuhair Shawush, akielezea uhusiano wake na Sheikh Shamsuddin.

Na ni jambo linalojulikana kuwa Sheikh Shamsuddin ni katika wanavyuoni wa Kishia wanaotambulika, na ni katika viongozi wakubwa. Na anatambulika kwa utunzi wake wa vitabu kama vile Asli ya madhehebu na historia zake. Na akaandika kwa ufasaha kuhusu ukhalifa na uongozi. Na akaeleza kwa undani mtazamo wa Mashia kwa ushahidi juu ya uongozi kutoka katika kizazi cha Mtume (s.a.w.w.) na mambo yanayowafanya wawe bora na kuwa mbali na madhambi. Akaandika kitabu (Nidhamu ya utawala katika Uislamu) kilichochapishwa mwaka 1373 H.

Na pia mwaka 1411 H. Na pia akaandika vitabu vingi juu ya fiqhi kuhusu (ijtihad za wanavyuoni na Taqlid) na pia (Al-Ihtiqar) na (Aljihad) na pia vitabu vitatu juu ya mapenduzi ya Imam Hussein na shughli wanazozifanya Mashia kila mwaka kwa kukumbuka kuuwawa kwake.

Nasisitiza kusema ya kuwa yeye kwa hakika (Sheikh Shamsuddin) ni mwanachuoni wa Kishia aliye dhahiri juu ya muelekeo wake, mwenye kudhihirisha maoni na fikra zake juu ya asli ya madhehebu na vigawanyiko vyake na mipango yake.

Kwa upande mwengine, hakika Sheikh Shawush ni mfuasi wa Salaf mwenye heshima. Na katika maneno ya mwisho niliyoyasoma kutoka kwake ni yale yaliyochapishwa na gazeti la Riyadh (Takriban 3891 tarehe 14 shaban 1424 H) kwa kuandikwa na Ustadh Rashin Muhammad bin Asaakir

chini ya unuani (safari ya maktaba ya Sheikh Zuhair Shawush Danashqiy maktaba kubwa ya kibinafsi katika ulimwengu wa kiislamu) na katika baadhi ya maneno:

"Sileti jambo geni katika kuueleza ulimwengu huu wa sasa, bali ni "Encyclopedia" ya elimu na ubora wake kwa warithi wa uislamu, na kuidhihirisha, kuipiga chapa na kuieneza.... Ambapo umefaidika umma kutoka kwa hazina ya ulimwengu huu kwa zaidi ya miaka 60 na bado ulimwengu unaendelea kutoa hazina hiyo kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, na kuilinda akida ya Salaf wema hadi leo.... Maktaba hii ina idadi kubwa ya vitabu vilivyoandikiwa kwa mikono vinavyofika 14,000 mbali na vile vilivyo chapishwa kwa mashine, na pia vile vinavyochukuliwa katika kuchapishwa kwa kiarabu ambavyo baadhi yake vinafika miaka 200.

Na kama alivyoandika juu yake Ustadh Badru bin Ali Twami. Mwanaharakati mwenye kusaidiana na wizara ya mambo ya kiislamu,waqfu, da'awa na uongozaji njia katika jarida (gazeti) la Riyadh yaliyochapishwa (idadi ya 12,929 tarehe 19 Ramadhan 1424 H) chini ya kichwa cha maneno. (Sheikh Zuhair Shawush na kuhifadhi kwake hazina asili za uislamu). Na katika baadhi ya maneno yaliyoandikwa humo.

("Mwanachuoni wa Hadith na Historia Sheikh Zuhair Shawush aliwasiliana na wanavyuoni wakongwe kwa kupokea mingi waliyoyaandika kwa upokezi wakufuatana. Na pia ni mwenye kutambulika mbele ya Sheikh wetu Abdulazizi bin Baaz (Mwenyezi Mungu amrehemu).... Mpaka akawa Sheikh wetu ni mwenye kurudi kwenye vitabu vyake (Zuhair Shawush) kwa kujua zaidi juu ya historia ya wanavyuoni wengi wa karne zilizopita. Alipata tuzo kwa upokezi wa hadith za Mtume (s.a.w.w.) na kwa utunzi wa vitabu vya kiislamu kati ya wanavyuoni wingi ambao nisingeweza kuwataja wote kwa udhuru?)

Huyu ni mwanachuoni mtukufu wa Salaf anaeleza juu ya uhusiano wake na Sheikh Shamsuddin, mwanachuoni shujaa

wa Kishia ili kuwa kama mfano unaofaa juu ya uhusiano unaostahili uwe baina ya viongo na wanavyuoni wa pande mbili hizi, pamoja nakuwa kila upande ni wenye kufuata misingi ya miongozo ya dhehebu lake.

Na ningependa kunukuu baadhi ya vipande na ushahidi katika yale aliyoyaandika mwanachuoni huyu wa Salaf juu ya uhusiano wake na Imam Shafi.

## MASHUHUDIO NA KUATHIRIWA MOYO KWA MAZURI

Katika mambo aliyoyaandika Sheikh Zuhair Shawush juu ya mambo aliyoyashuhudia kutoka kwa Sheikh Muhammed Mahdy Shamsuddin na kuathiriwa anasema :

"Ama baada ya hayo, Hakika Mwenyezi Mungu alinijaalia kuwa jirani na Sheikh Muhammad Mahdy Shamsuddin kwa muda wa miaka mingi. Na ninakumbuka baadhi ya matukio yenye kutujulisha hali yake katika maisha aliyokuwa akiishi." Kabla ya kukamilisha shughuli ya kununua jingo la kamati ya Shia karibu na nyumba yangu, alinitembelea Sheikh Shamsuddin akiwa na Sheikh Imam Sayid Musa Assadr nyumbani kwangu pindi waliponitukuza kabla ya kununua jingo hilo kwa kuniomba ujirani na kushirikiana nao. Na wao walikuwa wanadhani mimi niko kinyume na yale waliyonayo.

Na likanunuliwa jingo hilo na mafungamano kati yetu yakawa ya hali ya juu zaidi ya namna ujirani unavyo takiwa. Na ukaendelea uhusiano na tukawa tunapendana na kukirimiana.

Na ni jambo lisilofichika kuwa Sheikh Muhammad Mahdy ni mwenye kuwakilisha kamati ya Kishia iliyojuu katika Lebanon. Kwani yeye ndiye aliekuwa kiongozi wa kundi hili la dhehebu la Jaafariya ithna sharia katika akida na fiqh. Na hapo ndipo kukaanza utendaji kazi wa kielimu na vitendo kwa wafuasi wa dhehebu hili ambalo limekuwa ni lenye kutengemewa kwa upande wa mambo ya fiqh. Haya ni tangu kuanzishwa kwa madhehebu mengine ya kiislamu kama vile: Hanafi, Maalik, Shafi na baada yake ndipo likaja dhehebu la Imam Ahmad bin Hambali Mwenyezi Mungu amrehemu.

Na mimi nilikuwa ni mfuasi wa dhehebu la Imam Ahmad kwa akida na fiqh na ni mfuasi wa Salaf kwa desturi. Mwisho nikashikana na Sheikh al-Islam ibn Taimiyyah na Sheikh Muhammad bin Abdul wahab, yani kuwa muwahabi.

Na vitabu vingi katika maktaba yangu ni vyenye muelekeo wa upande wa uwahabi.

Na maana ya jambo hili ni kuwa hata kukiwa na tofauti kati yetu kubwa au ndogo, au hata kama kutakuwa na utengano kati yetu lakini.. na Mola anashuhudia sikuwahi kumsikia akinilaumu hata siku moja, wala kunipinga, wala majibizano. Haikuwa kwake yeye ila kuafikiana na sisi kwa kila tutakalolisema na ambalo ni la kweli katika dhehebu lake. Na haya yalikuwa ni kwa ajili ya utukufu wake na elimu yake na moyo wake mkunjufu.

Na siku moja alikuwa akihutubia katika hafla na maudhui yalikuwa yanahusiana na akida ya muutazila na Salaf na hayo ndiyo yenye tofauti kubwa. Akaeleza ile tofauti kama kwamba yeye ni mwenye kuleta mapatano na kwamba kila mtu afuate atakapo. Na wala watu wasiwatie wengine ima kwenye ukafiri, uovu wala kuwa ni wazushi (bidaa). Kisha akatoa ushahidi wa jambo hilo kwa maneno ya mshairi Ahmad Shauqi pindi aliposema: "kutofautiana kwa mawazo hakuharibu lolote katika mapenzi."

Na tulikuwa naye katika mkutano wa mjadala katika markaz al-bayaan. Na akazungumzia juu ya umuhimu wa kuungana na kuacha mambo yanayotutenganisha na kusema: "Nilikuwa Pakistan nikaona mahali kikundi cha Mashia, wanajipanga wenyewe kwa njia ambayo Mwenyezi Mungu hairidhii wala hakuiamrisha, kwa ajili ya huzuni wa Imam Hussein.

Na katika upande wa pili kuna kundi la watu wanamuomboleza Uthman bin Affan. Nikajuwa kwamba hawa wamefanya haya kwa muda wa siku kumi, nikamuomba Sheikh Abul-Hassan Nadwiy awape naswaha watu wake, Na mmoja aende anifikishie kwa watu wangu ya kwamba: Uthman Haridhii na wala Husein hayakubali matendo yenu haya.

Na akahutubu kwa kusema: "Na nyinyi vijana nyote. Nyinyi ni kizazi kipya, tubakieni katika kutenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (s.w.t.). Na huyu ndugu yangu Zuhair ni miongoni mwa vijana wa rika langu pia anayaunga mkono maneno yangu."

Na kwa mara ya pili aliutaja utawala wa Bani Uthman na akausifu na pia kuwasifu makhalifa wake. Kisha akaona kushangazwa kwa wengi katika wasikilizaji kwa vile walikuwa wanafahamu kuwa pana tofauti kati ya dhehebu lake na dhehebu la utawala wa Uthmania.

Kisha aliwazinduwa watu kwa kusema: "Mbona mmenyamaza na mlikuwa mkiyafurahia maneno yasiyokuwa hayo?... ufufueni utawala wa Uthmania, Waturuki tuliokuwa majirani katika daula moja. Na Mwenyezi Mungu aurehemu utawala wa Uthmania, kwani hatukufikwa na udhalili ila baada ya kuondoka utawala huo!!" watu wakapiga makofi na walikuwa katika mkusanyiko mkubwa sana.

Na mimi ninaamini ya kuwa maneno haya hayatoki ila kwa mtu mwenye busara na huruma, mjuzi wa siasa, na mwenye ujuzi kamili juu ya utukufu wa khilafa (uongozi), na umoja wa Waislamu. Sawa sawa na maneno ya kiongozi mwema Sayidna Ali bin Abi Talib pindi aliposema : "Ni lazima kuwe na dola, iwe mbaya au nzuri".

Kisha akayaeleza yale yaliyoyafika miji yetu ya kiarabu katika utengano baada ya kushinda viongozi dhidi ya Uturuki (Turkey). Na imefika wapi kadhia ya Wapalestina. Na akaeleza sana kwa undani juu ya mikasa inayotukabili.

Na wakati mmoja aliwasiliana nami nakuniuliza: "Je umeitwa kwenda Tehran?" Nikamjibu: "Bado! Na kwanini waniuliza hivyo?"

Akasema: "Huko ndiko kwenye kongamano juu ya kuleta umoja wa Waislamu na kuwaleta karibu watu wa madhehebu tofauti tofauti. Na wameitwa baadhi ya ndugu zetu wa kiSunni.. na wewe unastahiki kuhudhuria."

Nikamwambia: "Kama ningeitwa ningeenda" Akasema: Mimi sina uwezo wa kualika mtu lakini nitajaribu kuasiliana nao, pamoja na kuwa mimi na wao tunahitilafiana. Na nitawaeleza yale wanayopaswa kuyafanya, na kwa bayana hakuna mtu anayeweza kuongea katika kongamano hili juu ya

maudhui ya kuafikiana na kuhitilafiana vizuri kama wewe. (Huu ni utukufu wake nisioustahiki)."

Na siku ya pili walituzuru wahusika wa kongamano hilo kisha wakanialika na kutowa udhuru kwa kule kunisahau mara ya kwanza. Na wakanichangulia maudhui ambayo yangekuwa bora niyaandike. Na kwa hakika niliyaandika kwa haraka na nikamuonesha. Naye alikubaliana na yote niliyoyaandika.

Na Sheikh Shamsuddin ana mkono mrefu wa kuileta karibu miji ya Kiislamu. Lakini alikumbwa na baadhi ya matataizo katika shughuli hii,lakini bidii yake (na wafadhili wengine) ilileta matunda mazuri hasa kati ya nchi za kiarabu na utawala wa kiislamu wa Iran.

Vile vile msimamo wake katika kuleta mafungamano na mapenzi kati ya vikundi, mataifa na wakaazi katika nchi zote za kiarabu. Na ninakumbuka ya kuwa mikutano na kongamano nyingi zilizofanywa ni kupitia miongozo na mipango yake na hata kusaidia kipesa.

Na niliwahi kusikia kutoka kwa msimamizi mkuu wa kongamano la kiislamu la kitaifa ndugu Dkt. Ahmad Sidqy ad-dujan, na kutoka kwa naibu wa katibu ndugu Dkt. Muhammad Saleem al-uwaa, na wengine mambo mingi ya siri juu ya juhudi zake.

Na pia ningependa kueleza kwamba Sheikh Muhammad Mahdy Shamsuddin hata siku moja hakuwahi kubeba bunduki kwa kukabiliana na vijana wa mji wake na majirani wake, mbali na kuwepo kwa fitna ambayo imeendelea kwa muda wa karibu miaka 20. Na hayo yote ni kufuatia elimu na utendaji kazi kwake yeye kwa kila lililo katika kitabu chake hiki.

Na juhudi zake katika kuchangamsha mambo ya dini katika kila mji kama vile Syria, Lebanon na Misri.

Na wameshuhudia na kusadikisha jambo hilo majirani wake baadhi yao wakiwa ni manasara na pia Waislamu. Na lilikuwa jambo la kwanza katika kukutana kwa ni kutuliza mji.

Na jambo lenye kuhakikisha zaidi juu ya hali hii aliyokuwa nayo ni pale walipokusanyika wakubwa wa dini na madhehebu mbali mbali kwenda kumzuru yeye pindi alipokuwa mgonjwa. Na pia kutoa pole kwa Waislamu wote baada ya kufariki, kwani pole hiyo haikupewa familia na watoto wake tu kwani khasara ilikuwa imewakumba Waislamu wote kwa jumla.

Na katika maelezo ya kuleta mawazo kwa Sheikh Shamsuddin: Ni kuanzisha chuo kikuu alichokifanya kuwa huru na kujiunga kwa mwanafunzi wa dhehebu lolote la kiislamu, na pia madhehebu ya kikristo... Na akaifanya kamati ya usimamizi wa chuo kuwa ni watu kutoka madhehebu mbali mbali. Na jambo kubwa zaidi ni pale alipofanya muongozo wa masomo (sylabus) kuwa si wa dhehebu moja. Na walipomfuata wanafunzi wa dhehebu la Sunni wanaolala katika chuo kikuu wakati wa Ramadhani kwa kutaka kusali taraweh, aliwaambia : "Sisi hatuswali taraweh lakini kusanyikeni na mmoja wenu awaswalishe hiyo taraweh." Na hivyo ndivyo ilivyokuwa. Na jambo hili nilimsikia mwenyewe mbali na kwa wanafunzi.

Nikieleza tabia za Sheikh Shamsuddin, siku moja nilikuwa kwake, wakaja watu wakamshtakia dhulma walizotendewa... Na kabla ya kumaliza kuyasikiza malalamiko yao aliwapigia watu simu ambao sikuwatambua. Lakini ilidhihiri kutokana na maneno aliyokuwa akizungumza na idara ambayo ingeweza kutatuwa jambo hilo. Na katikati ya mazungumzo alieleza idara hiyo kama ambae amekasirika kwa kusema: Mimi nawafanya wao kama dhamana kwangu kwani hao ni majirani zangu, na wewe fanya vile unaona ni sawa kwa maoni yako" kisha akakata simu.

Na haukupita muda kukawa tena na mawasiliano ya simu, na ukadhihiri kuwa simu ile ilitoka kule alikokuwa akizungumza nako. Na baada ya maneno mafupi aliwaambia wale walioleta malalamiko : Nendeni hakika wamewasiliana nami wale wanaowadhulumu, na sasa hawatawadhulumu tena. Wakamshukuru Mwenyezi Mungu (s.w.t.).

Na ningependa kusema kuwa wale waliokuja kumlalamikia hawakuwa ni wafuasi wa dhehebu lake. Lakini walikuwa ni majirani zake alipokuwa akikaa karibu na chuo kikuu cha Salam, Beirut Mashariki.

Na ninamaliza utangulizi huu kwa kusema: Kwamba kuishi kwangu kote na Sheikh Muhammad Mahdy hakuwa yeye ila mwenye kutabasamu au mwenye uso mkunjufu wa furaha. Na anapokasirika basi haimchukui ila maneno kidogo tu kisha hurudi kama kawaida.

Na wala sikumuona yeye na yoyote katika majirani zake wa karibu au wa mbali ila ni mwenye kuishi nao vyema hata kama wanahitilafiana kidini au kimambo ya dunia. Bali nilikuta kila anaemjuwa huamiliana nae vizuri kama alivyosema Sayidna Ali (r.a) (mwenye maneno laini (matamu) yapaswa kumpenda).

Mwenyezi Mungu amrehemu Sheikh Muhammad Mahdy Shamsuddin Rehma nyingi, na atusamehe sisi na yeye. Na hakika ni cha Mwenyezi Mungu kile akitwaacho na ni chake kile akitowacho, na kila kitu kwake kina wakati wake. Sote ni wa Mwenyezi Mungu na sote kwake tutarejea. (Shamsu Din: Muhammad Mahdi kwenye mkutano wa miji ya kiislamu Uk. 14-29 Chapa ya mwaka 1424 (A. H.) - 2004 (A. D.)

Imebaki nieleze kuwa ulingano huu wa tabia za Sheikh Shamsuddin na jirani yake Sheikh wa Salaf, haioneshi kwamba kuna jambo lolote la kimaslahi au lengo la mambo ya kiulimwengu, kwani yuko katika daraja la uongozi (leadership) katika kundi kubwa miongoni mwa makundi ya Lebanon. Na Sheikh Zuhair Shawush alifanya utafiti na akawa mwanachuoni. Hakuwa na mambo ya kisiasa yanayomfanya aogopewe au ni mwenye kutarajiwa mbele ya Sheikh Shamsuddin.

Na Lebanon ni nchi wanaostarehe wakazi wake kwa kuwa na uhuru wa dini, wala haimtaki mtu awe ni mwenye kuficha imani yake au kufanya *taqiyah*. Haya yote ni kwa juhudi za Sheikh Shamsuddin.

Na kama vile juhudi za Sheikh Zuhair Shawush katika kuandika na kusimulia juu ya Sheikh Shamsuddin haielezeki ila ni uadilifu na kutekeleza wajibu, Mwenyezi Mungu amlipe mema.

## HAKUNA JAMBO KAMA KUISHI PAMOJA KWA MAISHAYA AMANI

Namna yatakavyokuwa mizozo ya Salaf juu ya Mashia au Mashia juu ya Salaf lakini wote wanaishi katika mahali pamoja (nchi,mji). Na wala haliwezi kundi moja kuliangamiza jengine. Na wala sidhani kama mawazo kama hayo katika pande mbili hizo. Wote kwa pamoja ni watu wa ardhi hii, wala haistahiki kwa moja kati yao kujiona bora juu ya mwengine kwa kutazama asili.

Ama juhudi juu ya kumfanya mtu abadili itikadi yake ima kwa kumfanya apende au kwa kumtishia aone upande mwengine sio sawa, imedhihiri kuwa juhudi hiyo imenowa. Pindi pale walipokuwa dhehebu la Salaf na uwezo mkubwa na likatumia pesa hasa pale uchumi ulipokuwa juu. Na zikamsahilishia yeye hali za kitaifa na mikoa wakati wa vita baridi (*cold war*) na pia mapambano ya mashariki na majeshi ya nchi za Mashariki hasa wakati wa vita vya Afghanistan. Ambapo ushia ulikuwa kwenye hali ya kuzingirwa kinchi na kimekuwa kama inavyojulikana.

Je waliweza Salaf kuleta mageuzi na mabadiliko katika itikadi ndani ya Ushia pamoja na kuwa waliweza kuathiri mipango ya elimu na njia za mawasiliano?

Sidhani kuwa wanaweza kudai lolote katika jambo hili, bali yalikuwa ni kinyume ya hayo ni kuzidi mapambano na kuzuka mielekeo yenye malingamano zaidi na Ushia.

Na alidhihirisha jambo hilo muusika mkubwa katika mambo ya kisiasa ambae alilingania kufanywa mjadala wa kitaifa baina ya madhehebu tofauti tofauti. Na yakaja mapendekezo juu ya mkutano wa kitaifa wa kwanza na wa pili ili kutilia mkazo juu ya jambo hilo. Na kulingania watu wote juu ya kuenea mijini na kukubali juu ya kuenea madhehebu mbali mbali na fikra tofauti.

Basi kuishi maisha ya amani ni chaguo la mantiki iliyosahihi wala hakuna badili yake ila kuenda mbio kwa ajili ya manufaa ya nchi, kuleta umoja wa jamii na kusaidia maadui kupata

wanayoyatarajia.

Na maisha ya amani hayatapatikana mpaka kuwe na usawa kati ya wananchi katika kupata haki na wajibu bila ya kubaguwa. Na pia kuwe na kuheshimiana pande zote na kutiana moyo.

Na hakika ninailingania nafsi yangu na wenzangu katika Mashia juu ya kujizuia na mambo yenye kuathiri. Na kuheshimu matendo ya ndugu wa Kisunni kwa kukomesha ovu lolote juu ya makhalifa na masahaba yanayofanyika kwa ajili ya ujinga au kupendelea. Na wajiepushe na matengamano.

Na kama ninavyowalingania ndugu zangu katika wanavyuoni na walinganizi wa KiSalaf na kila mwenye ikhlas miongoni mwao juu ya kuyaangalia kwa makini mambo wanayoyakazia sana juu ya ndugu zao Mashia. Hata kama watatofautiana nao juu ya mambo ya kiakida na fiqhi kwa dalili zinazo waridhisha, na kwa kufuatia jitihada za wanavyuoni wanazoziona kuwa ni hoja kati yao na kati ya Mwenyezi Mungu (s.w.t).

Basi inapaswa kukomesha kutoa fatwa za kutiana kwenye ukafiri na maneno ya kuchochoe ambao huenda yakaleta chuki. Na kubadilisha mambo hayo kwa kufanyia watu ulinganizi kwa Mola (s.w.t) kwa busara na kutumia maneno mazuri. Na kujadiliana kwa njia iliyo nzuri kama alivyoamrisha Mwenyezi Mungu (s.w.t).

Basi tunamuomba Mwenyezi Mungu azikusanye nyoyo zetu juu ya kumcha, na azifanya safu zetu ziwe ni moja kwa kheri, na ailinde miji yetu kutokana na machukivu na hatari. Na awaongoze wasimamizi wa mambo yetu, na awaafikie yale yatakayoleta manufaa kwa waja na miji. Hakika yeye ni mwenye kurehemu zaidi na shukrani zote ni za Mola wa viumbe wote.

## MJADALA, MAHALI PA MAKUBALIANO

Sheikh Hassan Safar katika mahojiano na 'Ilaf' ni mwenye matumaini ya kuwa watu wanaweza kuuondoa mushkili au tatizo la kutofautiana ki madhehebu.

Limefanywa jambo la kuleta umoja kati ya madhehebu ya Kiislamu ya Kishia na Sunni kuwa ni jambo muhimu ambalo linatembea ndani ya akili za Waislamu tangu kale hadi leo. Katika wakati ambao sauti zinatolewa na juhudi kufanywa kwa ajili ya kuleta umoja kuna baadhi ya mambo yanayokwenda mbio juu ya kuvuruga mipango hiyo.

Haya ni mahojiano na Sheikh Hasan Safar mmoja kati ya wale wanaovuma katika ulama wa mashia huko Saudia. *http://www.elaph.com*

Swali: Mwanzo ningependa kama mtatueleza juu ya tofauti kati ya kuwa na kushikamana na dini (*Tadayyun*). Kwa maana ni ipi tofauti ya mtu kuwa twaifiyyah katika fikra zake na kati ya kuwa mtu ni mwenye kushikamana na dini na pia kushikamana na dhehebu lake?

Jawabu: Kuwa na dini ni kule kushikamana mwanadamu na misingi ya dini na kufuata hukumu na maamrisho yake. Na utwaifiyyah ni kule kulemea mwanadamu kwa kundi lake na kutozifanyia usawa haki za makundi mengine.

Hakika katika chimbuko la dini la kimisingi ambalo halina upinzani baina ya madhehebu ni kule kushikamana na uadilifu. Yani kumpa kila mwenye kustahiki haki yake, awe Muislamu au kafiri bila ya kuangalia tofauti za kimadhehebu. Anasema Mwenyezi Mungu aliyetukuka (Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha kufanya uadilifu na hisani). Na akasema tena: "Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutowafanyia uadilifu." Fanyeni uadilifu huko ndiko kunakomkurubisha mtu na ucha Mungu.

Na hakuna dhehebu lolote katika madhehebu ya Kiislamu linaloruhusu kudhulumu na kuharibu haki za wengine, kwa

ajili ya kubadilisha dini au dhehebu. Na wale wanaotoa maoni maovu kwa wale wenye kutofautiana na dhehebu lao, huo uelevu na ufahamu mbaya au kueleza mambo yanayoleta chuki na uadui kwa kubagua. Au kwa ajili ya maslahi ya kibinafsi ambayo hayana mafungamano yoyote na dini au dhehebu lake.

Swali: Katika upande wa juhudi zinazofanywa kwa ajili ya kuleta ukuruba na uhusiano baina ya madhehebu ya Kiislamu katika UShia na USunni, kuna mambo kudumisha tofauti ziliopo na mizozo katika jamii. Je nyinyi ni wenye kuunga au kupinga jambo hili?

Jawabu: Hakika mimi ni mwenye matarajio ya kuwa jamii itaweza kuondoa mushkili huu wa tofauti za kimadhehebu kwa wakati huu tuliopo. Na nina matumaini kulingana na ukweli ufuatao.

Mosi: Kuzidi kima cha imani na uzingatiaji wa haki za watu, na pia kuweko kwa uhuru wa mawazo na wa kidini. Hilo ni kwa sababu mizozo ya kimadhehebu yanatokamana na kuziteka akili za watu na fikra zao, na kuwa fanya lazima waamini yanayofanya juu ya kuendeleza na fikra hii, na waipinge rai ile, na wafuate mwenendo huu na waepukane na njia ile.

Hakika kuwepo kwa mizozo hii kwa wafuasi wa madhehebu inawafanya wao kwa wao ni wenye kuhukumiana kuwa huyu ni kadha... na kuchunguzana kwa undani ki akida.

Lakini imani ikiwepo kwa kuheshimu haki za watu na kuheshimu uhuru wake wa kuchagua mambo ya dini na fikra aitakayo na iliyoyasawa, basi hapana mtu anayeweza kubadili cheo chake na kuleta mawazo yaw engine.

Anasema Mwenyezi Mungu (s.w.t): "Hakuna kutenzana nguvu katika dini." Na akasema tena: "Nyinyi mna dini yenu nami nina dini yangu (ninayoifuata)."

Naam, hapo kuna nafasi ya ulinganizi kwa yale anayoitakidi mwanadamu kuwa ni kweli, na kujadiliana, kutafiti, na

kutathmini na kurekebisha maoni na madhehebu katika mipaka ya kuheshimiana kwa pande zote mbili kama alivyosema Mwenyezi Mungu (s.w.t.): "Lingania katika njia ya Mola wako kwa kutumia busara na maneno mazuri na ujadiliane nao kwa njia iliyo nzuri."

**2.** Fursa za ujuzi na kupanua akili zimekuwa nyingi kati ya wafuasi wa madhehebu ya Shia na Sunni kupitia vitabu ni mijaladi *(volumes)*. Na mawasiliano ya ana kwa ana. Na kwa kuwezekana juu ya uhakika, hali ya kuwa mbali na kukifanya kuwa ni chenye kupotea au kukikejeli.

Hakuliona Imam wa msikiti au khatibu wa Husayniyah kuwa jambo hili ni njia pekee ya chanzo cha kupata maelezo na ukweli kutoka katika pande mbili hizi.

**3.** Umuhimu wa mapambano yanayoyakabili jamii ambayo yamepelekea jamii juu ya kuizunduwa, jambo ambalo linajenga umoja juu ya kujihusisha na wanajamii.

Basi kwa ukweli huu na mfano wake nina matumaini kuwa mambo yote yatakuwa sawa. Na kwamba yameanza kujitenga yale matatizo ya kutofautiana kimadhehebu.

Swali: Huenda katika tatizo sugu lenye kuleta tofauti kati ya Sunni na Shia ni vile msimamo wa Mashia juu ya Makhalifa na baadhi ya Sahaba. Je ni vipi tunaweza kutatua tatizo sugu hili?

Jawabu: Kupatikana uhusiano mwema kati ya Sunni na Shia sio lazima mmoja wao arudi nyuma juu ya maoni au rai yake. Mashia wana maoni yao juu ya maudhui ya Ukhalifa na Uimamu na kwamba hayo yako kwa ushahidi kutoka kwa Mtume (s.a.w.). Na wana ushahidi unao wafanya kuamini jambo hilo, na haiwezekani kwamba wao wanaweza kurudi nyuma juu ya mambo yaliyothibiti kwa dalili za kiakili na kisheria.

Lakini maudhui ya Khilafa na Makhalifa yamekuwa ni jambo la kihistoria. Basi ni kwa nini kizuizi kimekuwa kwenye njia

ya jamii hii ya wakati wa sasa? Ambapo wamekuwa Mashia hawana nafasi kwa ajili ya kuthibitisha maoni na rai zao. Au MaSunni wamekuwa na pupa juu ya kubadilisha na kutengua maoni ya Mashia juu ya jambo hilo.

Sisi sasa hatuko kwenye kuchagua baina ya Ukhalifa wa Abubakar au Ali mpaka tutilie muhimu juu ya kuridhishana kwa kuchagua moja kati ya hayo.

Lakini sisi tuko katika njia tofauti tofauti juu ya utukufu wetu katika ulimwengu huu. Je tupo au hatupo? Na ni upi muelekeo wetu kwa jamii katika ulimwengu huu wa sasa?

Haya ndiyo tunayotakikana sote kujishughulisha kwa ajili ya mafungamano na maisha yetu na mustakbali wetu.

Swali: Lakini mtazamo huu wa Kishia upande wa Khilafa umezuwa mambo yanayowatatiza wafuasi wa Sunni kwa kueneza maovu kama kuwatusi na kulaaniwa baadhi ya Makhalifa na Masahaba kwa upande wa Mashia?

Jawabu: Ikiwa ni haki kwa Mashia kuwa na maoni na rai zao basi si haki kwao wao kukosea dalili na mambo yanayotukuzwa na dhehebu jengine. Hilo linaleta kuenda kinyume na mafunzo ya dini na adabu. Na inapelekea kwenye fitina na kuharibu umoja wa Waislamu. Hivyo basi tunauchukulia ule uovu wa kuwatusi Makhalifa waongofu kuwa ni tendo la haramu na ovu. Halitokei ila kwa yule aliye mjinga au mwenye kupendelea upande mmoja. Na hakika wamewahi kuzungumzia juu ya tendo hili ovu wingi katika viongozi wa Kishia na wanavyuoni wao wenye kuleta amani.

Swali: Tatizo ni kuwa katika vitabu vya Mashia na matoleo yao mna maneno mingi katika kuwakosea Makhalifa na viongozi wengine wa KiSunni.

Jawabu: Vitabu vya kale vya Kisunni na Kishia vina tofauti juu ya mambo wanayotofautiana na pia kimadhehebu. Na vinaeleza juu ya hali za wafuasi wake.

Basi ni kwa nini tuwe mateka wa kufuata vitabu vya kale? Na kwa nini tunahukumiana sisi kwa sisi kwa ajili ya mambo yaliyopokewa kwenye vitabu vya kale?

Hakika ni juu yetu kupigana na jambo hili lenye giza linalotoka kwa watu wetu waliopita wa Kishia na Sunni. Na tutilie mkazo juu ya mambo yenye mwangaza ambayo yatatusaidia sisi kutengeza mambo yetu na kutatua matatizo yetu na kujenga umoja wetu na mapenzi. Maneno yenye kuchoma na matusi hayamo kwenye baadhi ya vitabu vya kale vya Shia, bali utayakuta kwenye baadhi ya vitabu vya kale vya Sunni. Kwa mfano wa kitabu cha Sunni cha Abdillahi bin Imam Ahmed bin Hambal (213-290 H) kimepigwa chapa nyingi ndani yake kuna mlango mzima karibu ya kurasa khamsini unaomkejeli Imam Abu Hanifa na kupendekeza kuchukiwa na kumsifu kwa uovu na pia kumshutumu na shutma mbaya kabisa. Je jambo hilo linamaanisha kuwa na mzozo na tofauti sasa baina ya wafuasi wa Hanafi na Hambali?

Na vile vile ukiangalia kitabu, *Tabaqat Shafiiyyah* utapata ndani yake maneno mingi ya kuchoma na utesi kati ya wanavyuoni wa dhehebu la Imam Hambali na la Imam Shafi.

Na katika vitabu vya Sheikh ibn Taimiah mna maneno mingi makali dhidi ya Mashia, viongozi na hata wanavyuoni wake.

Je tuendeleze madhara ya mizozo hii inayopatikana katika vitabu vya kale vya Sunni na Shia?

Swali: Baadhi ya nakala katika Internet mna maneno kutoka kwenu, ndani yake maneno maovu juu ya baadhi ya Makhalifa yanayokwenda kinyume na muongozo wenu wa kulingania umoja na uhusiano wa karibu kati ya madhehebu na kujitenga na maneno ya mizozo kutoka kwa waliopita.

Jawabu: Inaonekana kwamba njia hizi zinakereketwa na ile juhudi ya kuleta mapenzi na umoja wa kuwakurubisha Waislamu. Na kuleta hali ya kudhoofika kimadhehebu. Kwaajili hiyo zinaenda mbio kwa kutia shaka juu ya bidii na

juhudi zinazofanywa. Na sio tabu kuandika na kurikodi kaseti kwa wingi na kupenyeza baadhi ya maneno ndani yake.

Na ni muhimu kwangu mimi kueleza jambo maarufu kwamba nilikuwa nikiishi ndani ya upinzani wa kisiasa katika miaka ya thamanini baada ya kufaulu mapinduzi ya vita kati ya Iran na Iraq.

Na yalikuwa baadhi ya mawaidha yangu wakati huo ni juu ya siasa na madhehebu. Kisha tukagunduwa mapema dharura ya kuweka kando mfumo huu na kutumia mfumo wa huruma na mjadala na kutenda kazi kwa kuondoa tatizo la kutofautiana na kubaguana kimadhehebu.

Tulitangaza juu ya mabadiliko haya ya kifikra na siasa wakati huo na tulikuwa nje ya mji. Zikabadilika lugha zetu za kisiasa na kidini kufuatia mabadiliko yetu ya kuridhika. Na kisha kukawa na mjadala kati yetu na serikali na baadae tukarudi mjini kwa uwezo wa Mola. Na niliandika juu ya mambo haya (1410 H, 1989) kitabu kinacho zungumzia juu ya uhuru wa mwenye kuitakidi na *Attanawu'u wa atta'aayush* (uingi wa madhehebu na kuishi kwa amani), na kitabu *Tasaamuhu wa Thaqafatul-Ikhtilaf* (Uvumilivu kati ya wafuasi wa madhehebu na utakaso wa ikhtilaf) Na kitabu *(Ru'yatu haula sijali Madh-Habi* (maoni juu ya mashindano ya kimadhehebu).

Na pia nilitoa hutuba nyingi kwa wananchi wa Kishia katika sehemu niliyokuweko kwa njia ya mtandao wa *Internet* zilizobashiri juu ya mielekezo ya juhudi na kuvumilia na kuleta karibu. Nazo zinaeleza juu ya mambo tuliyoyaridhia, tunayoyaamini, na kuyatendea kazi.

Lakini baadhi ya wale wenye kulemea upande mmoja huenda wakatafuta maneno ya kuchochea kisiasa na kimadhehebu kutoka katika hayo tuliyoyaeleza na pia ndani ya maongozo ambayo tayari tumeyaepuka kimawazo na kuyatendea. Haya yote wanayafanya kwa ajili ya kubadilisha sura na kurudisha nyuma mbinu za kuleta umoja kati yetu.

Swali: Baadhi ya watu huenda wasione kuwa maelezo haya mapya kwamba ni namna ya maendeleo yanayojenga na kukomaa ki mawazo bali wao hufasiri kwamba hilo ni namna ya mbinu za kisiasa tu?

Jawabu: Maneno yanapokuwa ni juu ya undani wa nafsi na nyoyo basi sisi kama wanadamu hatuwezi kuyakubali au kuyapinga.

Kwa sababu hiyo ni sehemu hakuna aijuwae undani wake isipokuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t).

Na kimisingi haipaswi kwa upande wowote kutaka ushahidi juu ya ukweli wa upande mwengine kutoka kwao. Na wala hatudhani kama sisi tunahitajika kwa jambo hilo mbele ya kundi lolote.

Lakini kwa ajili ya wale wenye kupendelea upande mmoja tunasema kwamba mazungumzo ya kisiasa na ya kujuza yanaweza fasiriwa kwa kutumia mbinu za muda mbele ya mazungumzo ya kidini kwa watu wengi.

Swali: Ni yapi madhara ya twaifiyah (*confessionalism*) kwa nchi na mwananchi?

Jawabu: Twaifiyah (*confessionalism*) ni hatari kwa kila nchi au jamii kwa sababu zifuatazo:-

**1.** Unadhoofisha umoja wa wananchi na kuwa fanya watu wawe wenye kutiliana shaka wao kwa wao juu ya desturi badala ya kujifanya wao ni wenye umoja.

**2.** Unajenga uwanja wa mizozo na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

**3.** Inawakosesha baadhi ya wananchi faida ya mafundisho ya ukweli na uwezo pale wanaposhikamana na wajibu wao juu ya kutenda uadilifu.

**4.** Unawapa maadui nafasi ya kuchezea na kuharibu jambo hili la umoja na la kuleta maslahi ya nchi.

Swali: Ni zipi njia muafaka na zilizosalama juu ya majadiliano ya kimadhehebu ambazo zinaweza kuleta umoja na kumaliza *utwaifiyah* (kujitenga kimakundi)?

Jawabu: Njia muafaka za majadiliano yakimadhehebu ambazo ni muhimu ni kama:

**1.** Kukubaliana juu ya misingi ya kuishi kwa amani na kusaidiana kwa ajili ya manufaa ya nchi na jamii.

**2.** Kuchungua mambo yanayotutenganisha na njia za kuleta maelewano na kuzitilia mkazo.

**3.** Kujadiliana juu ya mambo yenye kutofautiana ili kujuwa dalili za kila upande na tegemeo la maoni yao na kujiweka mbali na maneno na tafsiri zilizo ovu.

**4.** Kuvisoma na kuvijua vita vilivyo sasa ambavyo vinaukabili Uislamu na jamii na kuleta suluhisho kifikra au kisheria kwa ijtihad za madhehebu tofauti tofauti.

## UHUSIANO WA MAFUNGAMANO BORA KATI YA SALAF (SUNNI) NA SHIA

Huenda wengi wakashangaa juu ya uwezekano wa kuwapo kwa utangamano mzuri kati ya Masalafi na Mashia, kwa kuwa kuna hitilafu kati ya pande mbili hizo katika masuala nyeti ya kiitikadi na kuwapo kwa historia yenye mambo mazito yaliyotokea, ambapo ni kawaida ya upande wa kisalafi kuwa na ukali juu ya mambo wanayoyaona kuwa yanaenda kinyume na itikadi zao. Si kwa upande wa Shia tu hata ndani ya masunni wenzao.

Lakini mimi nina matarajio mazuri na nahisi kwamba sasa kuna kukua kwa kifikra miongoni mwa pande za kiislamu zinazofanya kuwe na ukaribu wa kukubali kuwapo kwa maoni ya wengine na kuamiliana nao licha ya kuwepo tofauti kubwa nao.

Katika kukutana kwangu na kutangamana na wanavyuoni, wahubiri na wasomi wa kisalafi, nimehisi kuwa kuna mapya mazuri yanayojitokeza kwao wakiangalia maslahi ya dini na nchi na kujaribu kuchunga hatari zilizopo zinazowalenga wote.

Sheikh Hassan bin Musa bin bin Sheikh Ridha Saffar, amezaliwa mnamo mwaka (1377 A.H.) huko mjini Qatif, Mkoa wa Mashariki, nchini Saudi Arabia. Alipohitimu kusoma katika Chuo cha Qur'an, alijiunga na Madrasa ya msingi ya Zainul-Abidin, kisha akajiunga na Madrasa ya Kati ya Amin mjini Qatif, na hivyo kuanza kutoa khutba za kidini katika mwaka 1388 (A.H.) (1968 A.D.).

Mnamo mwaka 1391 (A.H.) (1971 A.D.), alikwenda huko mjini Najaf, Iraq kwa ajili ya kuongeza elimu na baadaye alikwenda kuendelea zaidi kwenye Hawza ya Qum (Iran).

Kisha alijiunga na Madrasa ya Rasuulul-Akram nchini Kuwait, na hapo ndipo alipokuwa ni miongoni mwa viongozi wa mwamko wa kiislamu nchini humo.

Sheikh Saffar amesimamia taasisi nyingi za kidini katika pande nyingi duniani ikiwemo Saudia, Oman, Syria, Iran na Marekani.

Vilevile ameshiriki katika matangazo mengi kupitia kwenye idhaa na magazeti mengi duniani. Ameshiriki mikutano mingi ya kiislamu ikiwemo Mkutano wa vijana wa kiislamu Marekani, na mkutano wa Umoja wa kiislamu chini Iran, pia vikao juu ya fikra katika Saudia; pia mkutano wa mlingano wa kuwa karibu baina ya madhehebu, nchini Bahrain.

Ametoa vitabu zaidi ya sabini na vimetarumiwa katika lugha mbali mbali za kigeni.

Sheikh huchukuliwa kama ni mmoja kati ya watu wanaopenda kuzungumzia uhuru wa kuwapo kwa wingi wa kiitikadi, na juu ya uelewa wa uzalendo na pia kufikia kuwa na neno moja katika Uislamu.